


## BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI



### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU WAOMBAJI WA NAFASI ZA MASOMO KWA NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi katika Vyuo ambavyo si Vyuo Vikuu ama Vyuo Vikuu Vishiriki nchini. Jukumu mojawapo la Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Hivyo, Baraza lina wajibu wa kuratibu udahili wa wanafunzi kwenye Vyuo na kozi/programu mbalimbali zenye idhibati ya mamlaka husika.

Baraza (NACTE), linapenda kuufahamisha umma kuwa udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kozi/programu zote zinazotolewa na Vyuo vya Elimu ya Ufundi umefunguliwa rasmi kuanzia tarehe **27 Mei, 2021 hadi tarehe 14 Agosti, 2021 katika awamu ya Kwanza.**

Hivyo, Vyuo vinaruhusiwa kupokea maombi ya udahili kuanzia leo tarehe 27 Mei, 2021 hadi tarehe 14 Agosti, 2021. Vyuo vitachagua waombaji wenye sifa kati ya tarehe 15 hadi 20 Agosti, 2021 na kisha tarehe **21 Agosti hadi 3 Septemba, 2021** majina ya waombaji waliochaguliwa yatawasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki. Majina ya waliochaguliwa na kuhakikiwa na NACTE yatatangazwa na Vyuo husika tarehe 16 Septemba, 2021 kwa ajili ya kuanza masomo tarehe 1 Novemba, 2021.

Aidha, waombaji wa programu za Afya kwenye Vyuo vya Serikali watatuma maombi yao moja kwa moja kupitia tovuti ya Baraza (NACTE) kuanzia leo tarehe **27 Mei, 2021 hadi tarehe 14 Agosti, 2021.** Majina ya watakaochaguliwa yatatangazwa tarehe **22 Agosti, 2021.**

Vyuo vyote vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi vitakavyopokea maombi ya wanafunzi kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada vinaelekezwa kuzingatia taratibu za udahili kama zilivyotolewa na Baraza kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Wahitimu wote wa Elimu ya Sekondari na Vyuo wenye sifa za kujiunga na kozi za Astashahada na Stashahada, wanashauriwa kufanya maombi yao kwa umakini ili kupata nafasi ya kujiunga na kozi/programu wanazozipenda na walizotimiza vigezo/sifa za kujiunga nazo kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Hivyo, Baraza linawashauri waombaji na wazazi kuhakikisha kuwa wanaomba kwenye Vyuo ambavyo vimeorodheshwa kwenye Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa mwaka wa masomo 2021/2022 (**Admission Guidebook for 2021/2022 Academic Year**). Mwongozo wa Udahili unapatikana pia katika tovuti ya Baraza ([www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz)).

**IMETOLEWA NA:  
OFISI YA KATIBU MTENDAJI  
TAREHE: 27/05/2021**